HOTUBA YA NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI,

NDUGU GEORGE M. MASAJU, KATIKA UFUNGUZI WA MAFUNZO YA WAENDESHA MASHTAKA JUU YA UENDESHAJI WA MASHTAKA YA RUSHWA NA UDANGANYIFU ULIYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA BENKI KUU YA TANZANIA DAR ES SALAAM

TAREHE 9 – 10 AUGUST 2011

Ndugu Washiriki wa Mafunzo,

Wakurugenzi Wasaidizi Divisheni ya Mashtaka,

Mawakili wa Serikali,

Waendesha Mashtaka,

Ndugu Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana

Itifaki imezingatiwa

Ndugu Washiriki,

Kwanza kabisa ninayo furaha kuwa nanyi leo hii katika mafunzo haya muhimu sana na kupata wasaa wa kuzungumza nanyi na pia kufungua mafunzo haya. Ninafahamu kwamba mafunzo haya yanayolenga katika kuwafunza namna bora ya kufungua na kuendesha mashtaka ya rushwa pamoja na yale ya udanganyifu. Natumaini mpo tayari kupokea mada zitakazowasilishwa katika mafunzo haya, na kushiriki kikamilifu.

Ndugu Washiriki,

Itakua sijatenda haki kama sitaipongeza timu iliyowaleta pamoja nyie washiriki kwa ajili ya mafunzo haya kwani wamefanya kazi kubwa hasa katika kutekeleza azma kubwa ya ofisi yetu ya kuendelea kujenga uwezo wetu wa kikazi.

Kujenga uwezo kupo katika mitazamo miwili mikuu. Moja, ni kuwa na rasilimali watu ya kutosheleza kukabiliana na ongezeko la kazi linaloongezeka siku hadi siku na pili rasimali watu hao kuwa na uwezo wa kutenda kazi zao kwa ufanisi wakimudu majukumu yao ipasavyo. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa ikipata ongezeko kubwa la kazi kutokana na mabadiliko ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa duniani, mabadiliko ambayo yameleta uchumi wa soko Huria katika mfumo wa Utandawazi .

Ndugu Washiriki,

Katika ofisi hii katika Divisheni ya Mashtaka, kwa mfano, kumekua na ongezeko kubwa la mashauri, uhalisia unaonyesha kwamba katika miaka ya hivi karibuni kutokana mabadiliko hayo ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa duniani pamoja na kukua kwa teknolojia makosa pia yameongezeka, hususan makosa ya Jinai ya kawaida nchini na makosa ya Jinai ya Kimataifa **(Transnational Crimes**) kama vile makosa ya utakatishaji wa Fedha (**money laundering**) Makosa ya Biashara ya Madawa haramu ya Kulevya (Drug Trafficking), Makosa ya Biashara ya Watu (Human Trafficking), Ugaidi (Terrorism), Uharamia baharini (Piracy), Rushwa (Corruption) , Makosa yanayotokana na matumizi ya Computer (cyber crimes), Makosa ya Kugharamia Uharamia (Terrorist financing) n.k. Katika ngazi ya Taifa Makosa ya wizi wa udaganyifu kwa kutumia nyaraka (fraud) na makosa ya Rushwa yameongezeka. Katika kukabiliana na uhalifu huo, Serikali imetunga upya sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007 ambapo sasa makosa ya rushwa chini ya Sheria hiyo yamefikia Ishirini na tano (25) kutoka makosa saba (7) yaliyokuwepo katika Sheria ya Zamani ya Rushwa. Vivyo hivyo Serikali imetunga upya Sheria ya Ukaguzi wa Mahesabu ya Umma **(The Public Audit Act, 2008**) ambayo pamoja na mengineyo imeleta ukaguzi wa kulinganisha kazi iliyofanyika na thamani ya fedha iliyotumika **(Value for money Audit)** pamoja na ukaguzi wa kitalaam wa Hesabu za maandishi ya kughushi **(forensic Audit).** Chini ya sheria hiyo mara tu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Fedha **(Controller and Auditor General**) anapojiridhisha na kuwepo kwa mazingira ya ujinai katika ukaguzi wake anatoa Taarifa kwa Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa, Polisi na Ofisi yako ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi za upelelezi na Mashtaka pale ushahidi unapothibitisha kutendeka kwa kosa la jinai la wizi wa fedha za umma.

Kwa kuwa mwelekeo wa adhabu za makosa mbalimbali yanayohusu mali kwa sasa duniani ni pamoja na urejeshaji wa mali zinazopatikana kutokana na uhalifu husika; na kwa kuwa sheria zetu kama vile Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, 2007; Sheria ya Uhujumu uchumi, 1984; Sheria ya Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu, 2006; Sheria ya Madawa ya Kulevya, 1997 pamoja na kuweka adhabu nyinginezo kama vile kifungo na faini pia zimeweka mkazo katika urejeshaji wa mali iliyopatikana kwa njia ya uhalifu, Ofisi yetu kwa kibali cha Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano imeanzisha kitengo cha Kurejesha na Uchukuaji wa mali

iliyopatikana kwa njia ya uhalifu kwa washtakiwa wanaopatikana na hatia ya makosa ya aina hiyo Mahakamani**. (Assets Recovery and Forfeiture Unit).** Kitengo hicho kipo katika Divisheni ya Mashtaka. Hii yote inamaanisha ongezeko la kazi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yote haya yakiashiria umuhimu wa ongezeko la rasilimali watu wenye ujuzi katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Hivyo umuhimu wa mafunzo zaidi kwa watumishi wa Ofisi hii ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Ndugu Washiriki,

Katika kukabiliana na changamoto hii ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeajiri Mawakili wa Serikali pamoja na watumishii wa kada nyingine ili kukabiliana na ongezeko hili la kazi linalokua kila kukicha. Pamoja na hayo Ofisi hii imefanya juhudi za dhahiri katika kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapeleka mafunzo/kozi fupi pamoja na ndefu watumishi wake ndani na nje ya nchi. Bila kusahau mafunzo ya papo kwa papo kazini **(on job training**).

Ofisi pia imeingia katika maelewano na vyombo na taasisisi mbalimbali ili viweze kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wetu, kama vile; **United Nations Office on Drugs and Crime (UNODC**) ambao wamesaidia sana kutoa mafunzo juu ya kuwalinda mashahidi **(witness protection),** kesi za uharamia na

"**cyber crimes**". Vilevile Ubalozi wa Marekani umewezesha Mawakili kupata mafunzo juu ya makosa ya kusafirisha binadamu **(human trafficking) Piracy, Terrorism Financing, Cyber Crimes**, **Money Laundering**. Bila kusahau Nchi ya Korea imejitolea kufundisha Mawakili wa Serikali kupitia mtandao kuhusu masuala ya **cyber crimes**, kumesainiwa mkataba wa maelewano juu ya kutoa mafunzo hayo ambayo yatatoka katika Chuo cha Makosa ya Jinai cha Korea **(Korea Institute of Criminology**). Mipango hii ipo katika hatua za mwisho kukamilishwa na matunda yake yataonekana katika siku za usoni. Kwa upande wao **United Nations Development Programme (UNDP)** wanawezesha mafunzo kuhusu Mikataba . Tunazishukuru Taasisi na Nchi ambazo wamekuwa wakitusaidai kujenga uwezo wetu kiutendaji katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Ndugu Washiriki,

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuwasomesha wafanyakazi mbalimbali stashahada ya uzamili, mafunzo mafupi kwa Makatibu Sheria, Secretaries, drivers, accountants, mawakili na wengine wanaendelea kusomeshwa pamoja na hayo ofisi inatoa ushirikiano kwa wale ambao wanapata nafasi za masomo bila kusomeshwa na ofisi kwa kuwaruhusu kuhudhuria masomo. Mafunzo mengine ni yale yanayoandaliwa na ofisi yenyewe kutokana na mahitaji ya kipindi hicho **(tailor made courses),** mfano mzuri ni kama mafunzo haya. Utaratibu wa kuwapeleka mafunzo wafanyakazi kila wakiajiriwa **(induction course**) umeanza tangu 2008 kwani ni muhimu kuwapa miongozo na jinsi ya kutimiza majukumu yao kwa ujuzi zaidi.

Ndugu Washiriki,

Kama vile ilivyo ada hakuna kitu kisichokosa changamoto, ongezeko hili la kasi ya majukumu katika Ofisi ya Mwanasheria mkuu wa Serikali linasababisha uhitaji mkubwa wa rasilimali watu. Upungufu wa rasilimali hiyo uko bayana. Kuacha hilo, pia baadhi ya Mawakili wa Serikali wenye ujuzi wamekua

wakiacha kazi bila kujali kwamba Ofisi imewasomesha au kuingia gharama ya kuwapeleka kozi mbalimbali. Waajiri wengine wamekuwa wakivizia kuajiri Mawakili wa Serikali kutokana na ujuzi wao mkubwa katika masuala ya sheria.

Kama nilivyosema hapo awali maendeleo ya kiuchumi yameleta mabadiliko mengi hivyo basi watu wanakimbilia sehemu nyingine wanazoamini wataneemeka kiuchumi zaidi. Wakati mwingine inakuwa watu hukosa uzalendo na kuelekea kwingine ambapo baada ya muda wengi huanza kukumbuka walikotoka kwani wakati wanaondoka walikuwa wanafikiria kuneemeka kimaslahi tu bila kutathmini mambo mengine yanayomzunguka hasa kukua kitaaluma jambo ambalo ofisi yetu inajivunia.

Ndugu Washiriki,

Nimeangalia ratiba yenu na kuona mambo mengi mazuri ambayo mtajifunza kama vile jinsi ya kufanya uchunguzi ambao ni tata, rushwa za kisiasa, uchunguzi wa makosa ya fedha, Uendeshaji wa kesi za utakatishaji fedha na rushwa Tanzania, Namna ya kupata vielelezo/kumbukumbu za ushahidi toka nje ya Nchi, Uendeshaji wa Kesi za wizi kwa njia ya udanganyifu wa matumizi ya Nyaraka, Matumizi ya Watoa Taarifa za uhalifu na namna ya kurejesha na kuchukua mali zilizopatikana kutokana na uhalifu na mengineyo ambayo yataongeza uwezo wetu wa uelewa na ufanisi katika utekelezaji. Naamini mtafurahia mafunzo haya.

Kama viongozi tungependa kuona kwamba ofisi hii inakuwa na rasilimali watu ya kutosha na yenye uweledi, kwa hiyo nitakazania mafunzo, hasa yale ya kazini (on job training) na yale ya kupanga (tailor made) kwa kuwa yanafundisha watu wengi. Pale rasilimali fedha inaporuhusu kuwafunza Mawakili wa Serikali na watumishi wengine katika maeneo maalum ya kazi zao nje ya nchi. Pia tutajitahihidi kuhakikisha vitendea kazi vinakuwepo

kuwawezesha wafanyakazi kukabiliana na changamsho zilizopo na kuendeleza uweledi wao.

Mwisho kabisa ninawataka na kuwashauri ya kwamba haya mtakayoyapata hapa yasiishie hapa bali muyafikishe kwa wengine ambao hawakupata nafasi ya kufika hapa na hasa hasa kuyaweka kwenye vitendo ambalo ndio lengo kuu la mafunzo haya. Ningependa sana kuona kwamba uwezo wetu wa kumudu majukumu yetu, unaenda sambamba na uadilifu katika utendaji wetu vinginevyo uwezo wetu hautokuwa na maana kwani tutakuwa tukitumia vibaya uwezo huo kwa maslahi binafisi badala ya kuzingatia Maslahi ya Taifa na Maslahi ya Haki. Tutambue tu kwamba kama tutatumia vizuri uwezo wetu wa kumudu majukumu (competence) tutachangia sana kudhibiti/kupunguza uhalifu nchini na hivyo kujenga amani ambayo ni chachu ya shughuli za kiuchumi zinazoleta maendeleo katika nchini. Kwa namna hii tutambue na kuzingatia kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nayo ni mdau muhimu katika kuleta maendeleo ya Kiuchumi nchini kupitia udhibiti wa uhalifu kwa njia ya mashtaka na Uandaaji wa Mikataba mizuri yenye maslahi kwa uchumi wa Taifa. Kwa hiyo, ni vyema Watumishi wa Ofisi hii tukawa na uwezo mkubwa wa kumudu ipasavyo majukumu yetu na kutumia uwezo wetu huo kwa uadilifu mkubwa kwa maslahi ya Taifa letu.

Baada ya kusema hayo natamka kwamba mafunzo haya yamefunguliwa rasmi. Nawatakieni kila la kheri katika utumisi wa umma.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.